JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS-TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI NYASA,

S.L.P 84,

MBAMBA-BAY.

Tarehe________________

Namba za simu:

Mkuu wa shule 0762054182/0783034008

Makamu Mkuu wa shule 0758430668

Patroni 0753188172

E-mail: nyasa.sekondari@nyasadc.go.tz

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi:_________________________

S.L.P__________________________________

Yah:MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYASA HALMASHAURI YA NYASA MKOA WA RUVUMA MWAKA 2024/2025

1. Utangulizi

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya CBG/HGK.

Shule ya sekondari NYASA ipo Mkoa wa Ruvuma,katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa.Ukiwa songea,utapanda magari yanayoenda moja kwa moja NG'OMBO kupitia Mbinga na Mbamba-bay.Tumia mabasi ya kampuni ya Kisumapai Express au Kangaulaya.Utashuka kituo cha CHIMATE kabla ya kufika NG'OMBO,na utapanda bodaboda hadi shuleni Nyasa Sekondari kwa nauli ya Tsh.1,000/=.

Shule ipo umbali wa Kilometa 35 kutoka mji wa Mbamba-bay,hivyo kwa wanafunzi wanaotokea Mbeya na Kyela wanaweza kutumia usafiri wa meli kulingana na ratiba hadi Mbamba-bay na kisha kupanda mabasi yanayoelekea NG'OMBO kutokea Songea au Liuli na kushuka CHIMATE.Hivyohivyo kwa wanafunzi watakao safiri kwa mabasi ya moja kwa moja kutoka Dar es salaam kuja Mbamba-bay.

Mwanafunzi atatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe__________hadi___________.

Edit with WPS Office

2. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1. Sare za shule

(i) Mwanafunzi anatakiwa awe na suruali mbili za kijani jeshi(Olive),zenye marinda madogo mawili upande wa mbele na mfuko mmoja nyuma,pana na zinazofunika viatu,ziwe na pindo la chini (turn-up).

(ii) Shati mbili nyeupe mikono mirefu,vishikizo vya kawaida (siyo chuma au shaba).

(iii) Sare za michezo ni bukta bluu (1),fulana bluu (1),track suit bluu (1) zenye michirizi myeupe na raba nyeupe.

(iv) Viatu vya ngozi vyeusi jozi mbili,visivyochongoka wala kuinuka kwa mbele na vyenye visigino vilivyoinuka kidogo.

(v) Soksi nyeupe (fupi) jozi mbili,zisizo na mapambo yoyote

(vi) Mkanda wa ngozi mweusi wa suruali wenye "buckle"ndogo

(vii) Ndala au sandals haziruhusiwi kuvaliwa na sare.

(viii) Aje na nguo za kazi ambazo ni suruali moja(1) ya khaki yenye marinda madogo mawili upande wa mbele na mfuko mmoja nyuma,pana na zinazofunika viatu,ziwe na pindo la chini (turn-up)

(ix) Tai mbili fupi za kijani jeshi(Olive) sawa na suruali.

(x) T SHIRT ya rangi ya samli(cream),zenye kola nyeusi (maarufu kwa jina la form six) aje mayo au anaweza kuipata shuleni kwa Tsh 15,000/=Kwa atakae hitaji

(xi) Aje na sweta rangi ya kijani jeshi (Olive)yenye shingo ya herufi V.

(xii) Vesti nyeupe mbili au zaidi.

(xiii) Vijana wa kiislamu waje na KANZU NYEUPE ya kuvaa msikitini siku ya ijumaa na sikukuu za Kiislamu.

NB:Nguo za nyumbani haziruhusiwi kuja nazo shuleni.

2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:

(i) Madaftari 12 quire 3 au 4;

(ii) Ream ya karatasi (A4) mbili (2) kwa mwaka;

(iii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa);

Edit with WPS Office

(iv) Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

(v) Scientific calculator kwa wanafunzi wanaosoma Basic Mathematics,Chemistry na Geograpy;

(vi) Godoro futi 2½×6

(vii) Mashuka Jozi 2 rangi ya bluu bahari,blanketi 1,foronya ya godoro 1,chandarua 1 rangi ya bluu au nyeupe;

(viii) Nguo za ndani za kutosha pamoja na taulo ya kuogea;

(ix) Vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kijiko na kikombe);

(x) Ndoo ndogo 1(lita kumi) yenye mifuniko;

(xi) Kwanja 1,jembe 1 (na mpini), mfagio wa nje 1 (chelewa),brashi ngumu 1 (hard broom),mopper 1;

(xii) Koti la maabara ( Lab. coat) rangi nyeupe kwa wanaosoma masomo ya sayansi;

(xiii) Jarada 1 (File) kwaajili ya kutunzia mazoezi na mitihani anayopewa na walimu;

(xiv) Sanduku gumu (Tranka) lenye kufuli kwaajili ya kutunzia vifaaa vyake;

(Xv) Aje na tochi au taa inayotumia nguvu za jua (solata)kwaajili ya dharula ya umeme.

NB:Vifaa kama vile magodoro,ndoo,madaftari,peni,Rimu,na vyombo vya chakula vinapatikana maeneo ya shule.

2.3. Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| Jumla | | 80,000/= |

Michango yote ilipwe benki kwenye Akaunti ya shule NMB 61701200143 NYASA SECONDARY SCHOOL.Shule HAITAPOKEA FEDHA TASLIMU.

Edit with WPS Office

Kabidhi risiti ya benki kwa Mhasibu ili upewe risiti ya shule pindi utakapofika shuleni.

### 2.4. Mambo mengine ya kuzingatiwa ili mwanafunzi aweze kusajiliwa:

(i) Nakala ya cheti cha matokeo ya kidato cha nne (result slip)

(ii) Nakala ya cheti cha kuzaliwa

(iii) Nakala ya cheti cha uraia kwa wasio Watanzania

(iv) Picha nne za passport zenye sare ya shule

(iv) Picha nne za wazazi na ndugu wa karibu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni

(v) Fedha za matumizi (pocket money) za kutosha,zitahifadhiwa kwa mkuu wa shule au benki.

(vi) Aje na fomu hii ikiwa imejazwa sehemu zote kwa usahihi.

MUHIMU:

*Kwa asiye na kadi ya bima ya afya aje na Tsh.50,400/=tu taslimu siku anapowasili ili ikatiwe kadi ya bima ya afya kwa mwaka mmoja.Gharama za matibabu ya mtoto ni za mzazi au mlezi mwenyewe.*

## 3. Sheria na kanuni muhimu za shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha,inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.Mambo hayo ni pamoja na ;

### 3.1. Sheria na kanuni za shule

(i) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;

(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

(iii) Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku ( Preparation);

(iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

Edit with WPS Office

(vi) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule;

(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

(ix) Kutunza mali za shule;

(x) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;na

(xi) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

ZINGATIA HAYA:

Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile,na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa.Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule ( Msiba au Ugonjwa).

3.2. Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na:-

(i) Wizi;

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo;

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

(vi) Kufuga ndevu;

(vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

(viii) Uvutaji wa sigara;

(ix) Uasherati,mahusiano ya jinsia moja,kuoa;

(x) Kusababisha mimba;

Edit with WPS Office

(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

(xii) Kwenda kwenye kumbi za starehe na nyumba za kulala wageni;

(xiii) Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

(xiv) Kudharau Bendera ya Taifa;

(xv) Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu;na

(xvi) Uhalifu wa mali ya umma kwa makusudi.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya nakuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA NYASA SEKONDARI

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli ( wizi kwa njia ya mtandao).Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE,NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:

Namba za simu:

| | |
|---|---|
| Mkuu wa Shule | 0762054182/0783034008 |
| Makamu Mkuu wa Shule | 0758430668 |
| Mwandamizi Malezi/Patron | 0753188172 |
| Mwandamizi Taaluma | 0768302730 |
| E-mail | nyasa.sekondari@nyasadc.go.tz |

................................

JOHN FESTO NDELWA

MKUU WA SHULE

Edit with WPS Office

4. Viambatanisho na Fomu Muhimu

4.1. FOMU YA KUKUBALI AU KUKATAA KUJIUNGA NA SHULE HII

4.1.1 Mwanafunzi

(i) Majina kamili (Matatu):________________________________________

(ii) Shule ya O-level aliyosoma:____________________________________

(iii) Namba ya mtihani (CSEE):_____________________________________

(iv) Tarehe ya kuzaliwa:___________________________________________

(v) Nakubali/Sikubali nafasi niliyopewa (Kata lisilohusika)

(vi) Nakili/Naahidi kutokumiliki au kutumia simu shuleni,kutoshiriki mgomo,fujo na makosa ya jinai.

saini ya mwanafunzi:______________________

4.1.2 MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

(a) Nakubali mwanangu apate elimu yake hapo shuleni

(b) Na kwamba afuate sheria na maelekezo yote,vinginevyo aadhibiwe

(c) Na kwamba mwanangu alelewe katika dini ya________________________

(d) Na kwamba siafiki yeye kumiliki au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule

(e) Na kwamba nitampa mahitaji yote yaliyoainishwa.

4.1.3 AFISA MTENDAJI WA KATA/KIJIJI/MTAA

Jina:____________________________________Kijiji/kata/Mtaa:____________________

Wilaya:__________________________________Mkoa:____________________________

Nathibitisha kuwa mwanafunzi____________________________________,____________

Edit with WPS Office

Ni wa kijiji/kata/mtaa huu na ni raia wa TANZANIA.

Saini na Muhuri:________________________ Tarehe:________________

4.2 TAARIFA KAMILI ZA MWANAFUNZI

4.2.1 Jina kamili:________________________________________________________________

4.2.2 Tarehe ya kuzaliwa:____________ Dini:____________ Dhehebu:_________________

4.2.3 Mahali ulipozaliwa:________________________________________________________

4.2.4 Shule ya msingi uliyosoma:______________________ Mwaka uliomaliza:__________

4.2.5 Shule ya sekondari uliyosoma:____________________ Mwaka uliomaliza:__________

4.2.6 Kidato unachokuja kuingia hapa:_____________________________________________

4.2.7 **Jina la baba/mlezi:**________________________________ Uhusiano:________________

Kazi ya baba/mlezi:_______________________________ Dini:______________________

Namba ya simu:________________________ E-mail:_______________________________

Anuani:________________________________ Namba ya nyumba:____________________

Kijiji/mtaa/kitongoji:_____________________ Kata:_______________ Tarafa:________

Wilaya:_____________________________ Mkoa:________________________

4.2.8 **Jina la mama/mlezi:**_________________________ Uhusiano:_____________

Kazi ya mama/mlezi:_________________________ Dini:__________________

Namba ya simu:_____________________ E-mail:_________________________

Anuani:____________________________ Namba ya nyumba:_______________

Kijiji/mtaa/kitongoji:_________________ Kata:______________ Tarafa:__________

Wilaya:______________________ Mkoa:______________________

4.2.9 Kazi yoyote ya uongozi uliyowahi kuifanya:

| MADARAKA/KAZI | MAHALI/SHULE | MWAKA |
|---|---|---|
| | | |
| | | |

Edit with WPS Office

| | | |
|---|---|---|
| | | |

4.2.10 Taarifa za ndugu wa karibu wamwanafunzi watakaoruhusiwa kuja kumtembelea mwanafunzi shuleni:

(i) Jina la ndugu:___________________________

Uhusiano:_________________

Mahali anapoishi:_____________

Namba ya simu:_______________

(ii) Jina la ndugu:_________________________

Uhusiano:___________________

Mahali anapoishi:__________________

Namba za simu:__________________

(iiii) Jina la ndugu:____________________________

Uhusiano:_________________

Mahali anapoishi:____________________

Namba za simu:____________________

(iv) Jina la ndugu:________________________

Uhusiano:___________________

Mahali anapoishi:___________________

Namba za simu:____________________

Nathibitisha kwamba,habari zilizotolewa hapo juu ni sahihi,naahidi kuwa na tabia njema,mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

Sahihi ya mwanafunzi:___________________ Tarehe:_____________

Edit with WPS Office

Edit with WPS Office